

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dar es Salaam
21 Aprili, 2026

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA AWEKA MWELEKEO MPYA, URASIMISHAJI SEKTA YA MAMA NA BABA LISHE NCHINI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amefungua Kongamano la Kitaifa la Mama na Baba Lishe Tanzania katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Rais Dkt. Samia amesema Mama na Baba Lishe ni mhimili wa uchumi wa wananchi, wakitoa huduma ya chakula kila siku na kuzalisha ajira zinazochangia ustawi wa familia nyingi mijini na vijijini.

Aidha, amesema Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kazi ili sekta hiyo ifanye kazi kwa usalama, tija na hadhi. Amezielekeza Wizara, Mikoa na Halmashauri nchini kote kutenga na kurasimisha maeneo ya biashara, kuboresha miundombinu, na kupanua mafunzo ya lishe, usafi wa chakula na uendeshaji wa biashara za Mama na Baba Lishe.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia amesisitiza matumizi ya nishati safi ya kupikia, akiitaja kuwa ni hatua ya kimkakati inayolinda afya, mazingira na ufanisi wa biashara za Mama na Baba Lishe, na kubainisha kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine kuhakikisha teknolojia na mifumo rahisi ya nishati safi ya kupikia inawafikia wananchi wengi zaidi.

Ameongeza kuwa, utekelezaji wa ajenda hiyo unaenda sambamba na Mkakati wa Taifa wa Uchumi unaoongozwa na maarifa, teknolojia na ushiriki wa wananchi, huku akihimiza amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa kama msingi wa shughuli zote za maendeleo.

Kwa upande wake, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima, amesema kongamano hilo linafungua hatua mpya



ya kutambua mchango wa sekta ya Mama na Baba Lishe na kutoa fursa ya kujadili changamoto, fursa na maboresho ya kisera na kiutendaji yanayowahusu.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila, amesema msukumo wa nishati safi unaotolewa na Rais Dkt. Samia una mchango mkubwa katika kulinda afya za wananchi na kuboresha mazingira ya kazi kwa kundi hilo la wajasiriamali, na kuipa sekta hiyo mwelekeo unaoendana na ajenda ya taifa ya maendeleo endelevu.

Akizungumza kwa niaba ya wadau, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Bi. Tully Esther Mwambapa, amesema taasisi za kifedha zitaendelea kushirikiana na Serikali kutoa elimu ya usimamizi wa fedha, mitaji nafuu na masoko kwa Mama na Baba Lishe ili kukuza biashara zao, pamoja na kuzalisha ajira kwa makundi mengine ya wajasiriamali.

Katika tukio hilo, Rais Dkt. Samia amekabidhiwa Tuzo ya Heshima ya Uhamasishaji wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia iliyotolewa na Umoja wa Mamalishe Tanzania (UMALITA) kwa kutambua uongozi wake katika kusimamia ajenda ya nishati safi nchini.

Aidha, Rais Dkt. Samia amekabidhi hundi ya **Shilingi 94,158,250,400** kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Prof. Riziki Shemdoe, kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kongamano hilo, lililowakutanisha washiriki kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, limebainisha msimamo wa serikali wa kuendeleza sekta ya Mama na Baba Lishe ndani ya ajenda ya uchumi jumuishi, afya ya jamii na maendeleo ya Taifa.



Bakari S. Machumu

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu